



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA BAJETI YA MANISPAA YA ILEMELA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela limeidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya **Shilingi Bilioni 71.57**.

Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 8.39** ni kwa ajili ya Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo, **Shilingi bilioni 45.29** ni Mishahara, **Shilingi bilioni 1.65**, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni 16.23** ni mapato ya ndani ambapo **Shilingi bilioni 8.76** kati ya fedha hizo za mapato ya ndani ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **shilingi bilioni Tshs 5.84** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi Bilioni 1.61** ni mapato fungwa.

Akisoma taarifa ya bajeti hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa, Ndugu Herbert Bilia ambae ni Mkuu wa divisheni ya Mipango na uratibu amevitaja vipaumbele **14** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambavyo ni kutoka Sekta za; **Afya, Elimu msingi na sekondari, utawala, miundombinu, ardhi, maendeleo ya jamii, biashara viwanda na uwekezaji, fedha kilimo, mifugo na uvuvi, TEHAMA, udhibiti taka na usafishaji, maliasili na uhifadhi mazingira pamoja na mipango na uratibu.**

Bajeti hii ya mwaka wa fedha **2023/2024** imepanda kutoka **Shilingi Bilioni 67.77** ya mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi bilioni 71.57** ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **5.6**.

Violencea S. Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
08 Februari, 2023

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,
Tovuti: www.ilemelamc.go.tz